

FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL 6

KISWAHILI PAPER 3 QUESTIONS

SEHEMU A (Alama 20)

SWALI LA LAZIMA

1. "Kusukuma kwa virungu tu inaweza kutupa picha mbaya..."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Bainisha tamathali moja ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

c) Waathiriwa wa virungu walifanya nini ili kujikwamua na hili lililowakumba? (alama 14)

SEHEMU B (Alama 20)

RIWAYA

2. "Wale mahabusu mkawafanyie kazi kama kawaida".

a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

b) Tambuau maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

c) Mbali na warejelewa ni kina nani wengine wanaoathiriwa na maudhui haya. (alama 12)

3. Jadili matumizi ya mbinu hizi riwayani

a) Sadfa (alama 10)

b) Barua (alama 10)

SEHEMU C (Alama 20)

HADITHI FUPI

4. "...Leo ni siku, siku ya nyani kufa na ambapo miti yote huteleza.."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Tambua mbinu mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

c) Eleza jinsi mzungumzajii alivyodhulumiwa. (alama 12)

5. Vijana wankumbwa na changamoto kadhaa katikauh maisha. Dhihirisha kwa mujibu wa kanda la Usufi. (alama 20)

SEHEMU D (Alama 20)

FASIHI SIMULIZI

6. a) Maigizo ni nini? (alama 2)

b) Tambua aina nne za maigizo. (alama 4)

c) Fafanua sifa nne za maigizo. (alama 4)

d) Eleza majukumu ya maigizo katika jamii. (alama 5)

e) Fafanua njia tano za kuendeleza fasihi simulizi katika jamii. (alama 5)

SEHEMU E (Alama 20)

USHAIRI

7.1. Natunga nikiwaasa, watoto kutowajiri, Nawaeleza hasa, ya mambo yaliyojiri, Ni kinyume shika sasa, huo ukweli mukiri, Komeni tena komeni, watoto kuwaajiri,

2. Wa ubwana kupigia, nyinyi mali kuzalisha, Migongo wamedandia, ya wana kutumikisha, Damuyo kujinyonyea, ili kujitajirisha, Komeni tena komeni, watoto kuwaajiri,

3. Tazameni majumbani, wakembe walea wana, Kuchuma chai shambani, kahawa pia ni wana, Mikono I mpinini, sagamba kuoteana, Komeni tena komeni, watoto kuwaajiri,
4. Mitaani wajuuza, mapeni kujipatia, Wazazi kwa mapuuza, uchuuzi kuwatia, Hoja maisha kukuza, huku wana wakundaa, Komeni tena komeni, watoto kuwaajiri,
5. Nako huko madukani, magunia kusombeshwa Ya nafaka masikini, maisha kuzoroteshwa, Watoto wapatieni, nafasi kusitawishwa, Komeni tena komeni, watoto kuwaajiri,
6. Hata nako viwandani, vikembe wameingizwa, Ati uanagenzini, talumani waingizwa, Ni haramu sikizeni, wana ajira kuingizwa, Komeni tena komeni, watoto kuwaajiri,
7. Ni kinyume kisheria, kuziponda zao haki, Wana wanazo sikia, watoto hawajiriki, Serikali takutia, gerezani tajutia, Komeni tena komeni, watoto kuwaajiri,
8. Mahali pa wana kuwa, wende shuleni kusoma, Ajira isiyo sawa, kabisa ipate koma, Ndipo wataweza kuwa, taifa lije watuma, Komeni tena komeni, watoto kuwaajiri,

Maswali

- a) Lipe shairi anwani mwafaka. (alama 1)
- b) Eleza muundoi wa shairi hili. (alama 4)
- c) Taja sehemu mbalimbali ambapoi watoto hutumikishwa. (alama 2)
- d) Tambua toni ya shairi hili. (alama 2)
- e) Ni nini dhamira ya mshairi kutunga shairi hili. (alama 2)
- f) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- g) Taja kwa kutoa mifano mwafaka jinsi mtunzi alivyotumia uhuru wa kishairi. (alama 2)
- h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi hili (alama 3) Nikiwaasa Kusombeshwa Kuziponda zao haki